

**Tangu Sasa Na Kuendelea Hatumchukulii
Mtu Kwa Jinsi Ya Mwili**

**(From Now On We Regard No One
According To Flesh)**

Na

John Kombo

**Tangu Sasa Na Kuendelea Hatumchukulii
Mtu Kwa Jinsi Ya Mwili**

**(From Now On We Regard No One
According To Flesh)**

Na

John Kombo

June 24, 2014

Tangu Sasa Na Kuendelea Hatumchukulii Mtu Kwa Jinsi Ya Mwili

Jana nilikuwa nasoma Biblia yangu nilipofungua 2 Wakorintho 5:16. Katika msitari huu Paulo anaandika, *“Hata imekuwa sisi tangu sasa hatumjui mtu awaye yote kwa jinsi ya mwili. Ingawa sisi tumemjua Kristo kwa jinsi ya mwili, lakini sasa hatumtambui hivi tena.”* Alafu nikakumbuka barua iliyonitia moyo niliyoipata kwa ndugu Paulo Warford. Aliandika, *“Furaha yangu kuu na faraja ni kutambua kuwa maisha haya ni ya muda mfupi na kwamba siku fulani, nitamuona mwanangu tena na hakuna kitakachotutenganisha tena kwa sababu hakuna kuwa na kifo tena wala machozi. Ninatarajia kwamba unaweza kurahia pamoja nami furaha hii kwa sababu siku fulani utapata kumuona kijana wako tena. “Ndiyo, hayo ni maneno yanayotia faraja kwamba mahitaji ya Wakristo wanaoamini ni kusikia au kuambiwa.*

Kitu kimoja pekee ndo kiko wazi kutokana na kauli ya Paulo, anatamani kwamba tuondoe mawazo yetu kimwili na tutafute kumfahamu kila mmoja katika Kristo zaidi sana kuliko mambo yaliopo katika ulimwengu huu. Tunapaswa kutafuta kumfahamu kila mmoja wetu kulingana na uhusiano wetu wa kiroho tulionao ndani ya Kristo Bwana, Yesu Kristo hayupo tena nasi kimwili, lakini tunamfahamu kiroho. Ndugu zetu, watoto, na jamii waliokufa katika Kristo hawapo tena nasi kimwili. Tunawafahamu na tunaweza kuwakumbuka kana kwamba wako nasi leo. Mtoto wa ndugu Paulo aliyefariki miaka 4 iliyopita bado anaishi naye;kijana wangu aliyefariki mwezi mmoja uliopita bado anaishi nami leo pamoja na mke wangu Florence. Tunafuraha na kufarijiwa kwamba siku moja tutakuwa pamoja na hakuna kitakachotutenganisha.

Paulo anatia moyo, *“Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi.”* (Kol. 3:2). Biblia inatupatia maelekezo kuhusu tulipotoka. Inaonyesha sisi ni wakina nani na tunakwenda wapi. Unaweza kuuliza, *“Kwa nini tuko hapa?”* Kufahamu ni kwa nini tupo hapa ni kuelewa kwamba tunaelekea kwenye umilele nah ii inaleta maana kwa kile tunacho kifanya hapa duniani. Hii *“habari njema”* inaweza kupatikana tu katika kitabu, *“Biblia”*

Neno la Mungu hutupa uhakika kwamba kuna maisha baada ya kufa. Hii huleta maana katika maisha kabla ya kufa. Kama hakuna uzima baada ya kufa, basi maisha hayana maana katika dunia. Tunapaswa tu kula, kunywa, na kufurahia maisha mafupi tuliyonayo. (1 Kor. 15:12-19).

Tunamwamini Mungu anayeweza kutukirimia zaidi ya dunia hii. Vinginevyo kusinge kuwa na Mungu na tungepoteza muda wetu

kumwabudu Mungu ambaye hayupo. Injili ni habari njema. Ni habari njema kwa sababu Yesu alikufa, na akazikwa, na kwamba alifufuka katika wafu (1 Kor. 15:1-4)

Mungu awabariki.

John Kombo

